

Jina _____ Nambari _____

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

SAA: 2 ½

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2010 WILAYA YA MASAKU

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari

KISWAHILI

KARATASI YA 3

SAA: 2 ½

Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

LAZIMA

FASI DI SIMULAZIONE

1. Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali

Hapo zamani za kale, Murungu (Mungu) alimtuma kinyonga kwa watu. Alimwambia "Nenda kwa waja wangu na uwaeleze kuwa mту akifa, awekwe nyuma ya nyumba na baada ya siku mbili atafufuka."

Kinyonga akaanza safari. Alitembea polepole akapanda milima na kuvuka mabonde. Njiani akakutana na sungura. Sungura akamuuliza, "Unaenda wapi kinyonga?" Kinyonga akamjibu, "Naenda kwa watu kuwapelekea ujumbe kutoka kwa Mungu kuwa mtu akiaga dunia awekwe nyuma ya nyumba kwa muda wa siku mbili kisha ataweba kufufuka."

Sungura hakufurahia jambo hilo. Akamwambia kinyonga kwa vile ana mbio, amwachie jukumu hilo apeleke ujumbe huo kwa watu. Kinyonga hakukubali. Hivyo sungura alimwacha kinyonga na kuchana mbuga.

Sungura alikimbia kukurukakara hadi kwa watu. Alipowasili alimwambia "Nimetumwa na Mungu," Watu waliposikia hivyo, wakafungua masikio yao. "Nimeambiwa na Mungu kuwa mту akifa, afe alale na kuzikwa mara moja." Nusura watu wamuue kwa kuleta ujumbe huo. Wengine walitaka kumfanya kitoweo lakini sungura akatoroka.

Sungura akiwa njiani kurudi alimwona kinyonga kwa mbali. Akajificha kichakani. Sungura alisukuma jiwe kubwa akielekeza alikokuwa kinyonga. Jiwe lilimwangukia kinyonga pu! Na kumuua papo hapo.

Sungura alipofika kwa Mungu na kumweleza aliywaaambia watu, Mungu alikasirika ja mkizi. Alimvuta masikio yakawa marefu na kumwonya asiseme uwongo tena. Kinyonga hakufikisha ujumbe. Watu waliamini ujumbe wa sungura. Mpaka sasa watu huamini ujumbe ulioletwa na sungura.

Maswali

- Maswali

(a) (i) Hii ni hadithi ya aina gain? (alama 1)
(ii) Toa sababu. (alama 1)

(b) Taja sifa zinazoitambulisha hadithi hii kama fasihi simulizi. (alama 3)

(c) Taja maudhui ya hadithi hii. (alama 3)

(d) Taja aina mbili za matumizi ya lugha kwenye hadithi. (alama 3)

(e) Hadithi hii ina umuhimu gani katika jamii. (alama 4)

(f) Eleza nyimbo hizi (alama 3)
(i) Bembelezi
(ii) Wawe
(iii) Nyiso

(g) Taja sifa zozote za vitendawili. (alama 2)

RIWAYA

UTENGANO: SAID A. MOHAMED

Jibu swali la 2 au la 3

2. "Nisingekutenda nilivyokutenda la lakini baada ya kisa mkasa"

- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
(b) Kisa kinachorejelewa hapa ni kipi? (alama 12)
(c) Eleza sifa za anayeambiwa. (alama 4)

3. “Wanawake katika riwaya ya utengano wamepewa nafasi duni katika jamii.” Thibitisha kauli hii kwa kutolea mifano. (alama 20)

TAMTHILIA **KIFO KISIMANI : KITHAKA WA MBERIA**

Jibu swalii la 4 au la 5

4. Tamthilia ya Kifo Kisimani inaeleza uhalisi wa mambo yalivyo barani Afrika.
Thibitisha kauli hii. (alama 20)
5. Eleza wasifa wa wahusika wafuatao kisha uonyeshe umuhimu wao katika tamthilia ya Kifo Kisimani.
(a) Gege
(b) Atega (alama 20)

HADITHI FUPI

Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi nyingine K.W. Wamitila

Ngome ya nafsi : Na Clara Momanyi

6. (a) Eleza kwa kina masaibu yaliyomkumba Naseko. (alama 8)
(b) Je, masaibu hayo yalitokana na nini? Fafanua (alama 6)
(c) Eleza sifa za Naseko. (alama 6)

USHAIRI

7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali

Sema semea wajibu, ewe mwenye kutetema,
Sema na walo karibu, na wa mbali ukisema,
Sema kufunza wajibu, werevu au hekima,
Sema asikie nani, mlimwengu asokoma.

Sema yanayokukaa, yaliyo kukusakama,
Sema yaliyozagaa, uwambie kuungana,
Sema unajihadaa, wadhani yatawafuma,
Sema asikie nani, usigejua kusema.

Sema semea uasi, na hizi nyingi zahamu,
Sema na wasiwasi, utarajie salama,
Sema neno la risasi, lipenyalo likiuma,
Sema asikie nani, usiyejua kusema.

Sema bila ya ukali, bembeleza ukisema,
Sema neno la asali, wataramba wakutema,
Sema tumia akili, kwao huikosi shutuma,
Sema iwe jambo gani, mlimwengu asokoma.

Sema zitaje ghururi, dunia ni kama dema,
Sema haiweke siri, inavuja ikitema,
Sema dunia hatari, mtendayo yafuuma,
Sema ajaliye nani, mlimwengu hao wema.

Sema na katu sisemi, kwa asojua kupima,
Sema awe ni mtemi, asojua nilosema,
Sema miko yangu mimi, sisemi neno daima,
Sema niseme na nani, ili iweko salama.

Maswali

- (a) Taja na ueleze aina nyingine tatu za bahari za shairi hili bali na tarbia. (alama 6)
- (b) Toa mifano miwili ya maneno yalioandikwa kishairi na kisha uyaandike kisanifu. (alama 2)
- (c) Toa mifano mwafaka kushuhudia kuwa shairi lina ujumbe wa kukatiza tamaa. (alama 4)
- (d) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
- (e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumika kwenye shairi
 - (i) Yaliyozagaa
 - (ii) Dema
 - (iii) Ghururi
 - (iv) Zahama(alama 4)